# Je, Mifupa mikavu yaweza kuishi?

# UNABII



PASTOR JAMES KALEKWA

# Je, MIFUPA MIKAVU YAWEZA KUISHI?

-Unabii-

James Kalekwa

*Ezekieli 37:1-3SUV "Mkono wa Bwana ulikuwa juu yangu, naye akanichukua nje katika roho ya Bwana, akaniweka chini, katikati ya bonde; nalo limejaa mifupa; akanipitisha karibu nayo pande zote; na tazama, palikuwa na mifupa mingi katika ule uwanda! Nayo, tazama, ilikuwa mikavu sana. Akaniambia, Mwanadamu, je! Mifupa hii yaweza kuishi? Nami nikajibu, Ee Bwana MUNGU, wajua wewe."*

# Salamu za Mama Mchungaji JK.

Juni 20, Mungu alitupa zawadi ya maisha ya mtumishi wake Pastor JK, mtu wa juhudi nyingi katika Kristo na maarifa ya kimungu. Kwa muda ambao nimekuwa naye kwenye maisha, nimemtambua kama mtu anayempenda Mungu kiasi cha mimi kukosa neno la kuelezea. Huyu ni mtu aliuzwa kwa Mungu na utumishi!

Amewekeza muda mwingi kuandika mfululizo wa vitabu hivi vya kielektroniki ili avitoe bila malipo kama sehemu yake ya ujenzi wa mwili wa Kristo… kwa niaba yake, ninaomba ukipokee kwa kuthamini dhabihu! Ninakuombea ya kwamba maisha yako yanageuzwa kwa kitabu hiki kimoja tu kwa jina la Yesu Kristo.

Pili, ninaomba uwasambazie kitabu hiki watu wengi zaidi ili maono ya kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari yatimilizwe.

Na hatimaye, kwa kuthamini zawadi ya mtu huyu wa Mungu, muombee, mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumsherehekea ukimweleza namna gani umesadika na utumishi wake – itafaa sana.

Heri ya siku ya kuzaliwa mume wangu mpenzi. Heri ya kuzaliwa Pastor JK – zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu!

Frida James Kalekwa (Mama mchungaji JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2025
Dodoma, Tanzania

# Maana ya Unabii

Ni tendo la kuyatangulia mambo yajayo na kuyapa muelekeo wa namna yanapaswa kuwa kwa kuuendea ulimwengu wa roho na kuusemesha , nikusema na kesho yako ukiwa bado unaishi leo.

# Mambo muhimu kujua kuhusu unabii

## Lugha ya Unabii

Ni vizuri kujua unabii ni jambo la kiroho na linapatikana katika ulimwengu wa roho. Kufaidi na kuvuna yale yaliyo kwenye ulimwengu huo inadai ufahamu kuhusiana

na ulimwengu huo. Huwezi kuyaelewa na kuyapambanua kwa ubaya wake mambo ya ulimwengu wa roho (ambamo ndimo unabii ulipo) na lugha zinazotumika huko. Ukweli ni kwamba kuna mambo zaidi ya yanayoonekana hivyo inahitaji kuielewa lugha ya ulimwengu wa roho ili kuyaelezea na kuyaendea mambo hayo.

Hapa ninamaanisha, unaweza ukasikia au ukaona neno “mkono” katika ulimwngu wa mwili na lugha ya mwilini. Hata hivyo, mkono ikawa ni lugha inayowasilisha jambo jinginelo katika ulimwengu war oho na lugha za unabii.

**Mambo ya msingi kuhusu ulimwengu wa Roho**

Ulimwengu wa roho ni halisi na sio habari za kufikirika (sio myth) na uhalisia wake ni kuwa;

1. Ulimwengu wa roho ndio chanzo cha ulimwengu wa mwili. Ni ukweli wa kimantiki ile ya kwamba kitu fulani kipo ni uhalisia kuwa kuna kitu kimesababisha hicho kitu kuwepo. Uwepo wa kitu fulani ujumbe ya kuwa kuna mahala kimotokea na kimetokana nacho.

Mfano rahisi ni huu, ile ya kwamba mimi nipo na unaweza ukabarikiwa na huduma na utumishi niliobeba… ikupe ujumbe ya kwamba nina baba na mama; nina wazazi… ninatoka kwao na ninatokana na wao! Ile ya kwamba huwajui, hujawahi kukutana nao… Usiwahi kudhania ya kwamba sina wazazi! Uwepo wangu ni uthibitisho wa uwepo wa wazazi wangu!

Ingawa wewe haujui hivyo kwa ushahidi unaoshikika lakini ile ya kwamba ulimwengu wa mwili upo ni ushahidi kwamba ulimwengu wa

roho upo pia ambao ndio chanzo cha ulimwengu huu unaoonekana.

*Mwanzo 1:1SUV "Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi."*

Huo mwanzo unaozungumzwa hapo ni wa ulimwengu wa mwili na si mwanzo wa Mungu. Kwa hiyo, ni salama kusema Mungu alikuwa kabla ya mianzo… na kwa kuwa Mungu ni roho, basi alikuwepo katika ulimwengu wa roho!

2. Ulimwengu wa roho ulikuwepo kabla ya ulimwengu wa mwili na utakuwepo hata baada ya ulimwengu wa mwili kwa sababu ya ukweli

kwamba kuna siku huu ulimwengu wa mwili hautakuwepo tena.

3. Ulimwengu wa roho una nguvu zaidi ya ulimwengu wa mwili; kwa sababu hiyo ulimwengu wa roho unautawala ulimwengu wa mwili, ili kutoa vitu kwenye ulimwengu wa roho kuleta mwilini inahusisha kutabiri au kutoa unabii.

4. Ulimwengu wa roho upo sasa, ulimwengu wa roho sio tu kuhusiana na mambo yajayo “futuristic”; kuwa na mtazamo huu utakuzuilia

kunufaika na uwepo wa ulimwengu wa roho na utendaji wake sasa.

5. Ulimwengu wa roho una mfumo wake wa mawasiliano unaofahamika na kueleweka. Hata kama kuna vitu vimeitwa siri bado hueleweka kwa sababu Roho wa Bwana huyafunua mambo yote na hatimaye yanaeleweka.

*1 Wakorintho 2:10-11SUV "Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu. Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu*

*iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu."*

## Mfano wa lugha za ulimwengu wa roho

Kwenye nadiko letu nanga kutoka kwa nabii Ezekieli, kuna maneno yanayotumika kuelezea nini kinaendelea ndani ya unabii huo ambayo kimsingi yanavyosikika katika ulimwengu wa mwili, si yalivyo katika uliwengu war oho.

Maneno yanayotumika ni kama yafuatayo:

- *Mkono wa Bwana ulikuwa juu yangu*
- *Akanichukua katika roho ya Bwana*
- *Akaniweka chini*

- *Akanipitisha*

*Ufunuo wa Yohana 1:9-11SUV "Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo,* ***nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo****, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu.* ***Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana****; nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu, ikisema, Haya uyaonayo uyaandike katika chuo, ukayapeleke kwa hayo makanisa saba: Efeso, na Smirna, na Pergamo, na Thiatira, na Sardi, na Filadelfia, na Laodikia."*

Unaona hapa Mtume Yohana anaonyesha alikuwa Patmo kisha anaonyesha tena alikuwa katika Roho. Sasa huko katika Roho anasikia sauti ya baragumu… Kumbe katika roho kuna milio, kuna sauti! Kinachonifurahisha ni kwamba hiyo sauti kama ya baragumu ndiyo ilikuwa inaongea na kutoa unabii kwa makanisa saba.

Fikiria unasikia mtu anaongea ila ni kwa sauti baragumu! Huenda sijafika mahali pazuri kiufahamu kuweza kuelewa vya kutosha kinachowasilishwa hapa. Sasa zingatia hili, inasikika sauti tu ya baragumu ikitoa ujumbe – inafikirisha sana!

Huko kwenye ulimwengu war oho kuna shughuli nyingi sana.

*Zaburi 18:6-16SUV "Katika shida yangu nalimwita Bwana, Na kumlalamikia Mungu wangu. Akaisikia sauti yangu hekaluni mwake, Kilio changu kikaingia masikioni mwake. Ndipo nchi iliyotikisika na kutetemeka, Misingi ya milima ikasuka-suka; Ikatikisika kwa sababu alikuwa na ghadhabu.* ***Kukapanda moshi kutoka puani mwake****, Moto ukatoka kinywani mwake ukala, Makaa yakawashwa nao.* ***Aliziinamisha mbingu akashuka****, Kukawa na giza kuu chini ya miguu yake.* ***Akapanda juu ya kerubi akaruka****, Naam, aliruka*

*upesi juu ya mabawa ya upepo.* ***Alifanya giza kuwa mahali pake pa kujificha,*** *Kuwa hema yake ya kumzunguka. Giza la maji na mawingu makuu ya mbinguni. Toka mwangaza uliokuwa mbele zake Kukapita mawingu yake makuu. Mvua ya mawe na makaa ya moto.* ***Bwana alipiga radi mbinguni, Yeye Aliye juu akaitoa sauti yake****, Mvua ya mawe na makaa ya moto. Akaipiga mishale yake akawatawanya, Naam, umeme mwingi sana, akawatapanya. Ndipo ilipoonekana mikondo ya maji, Misingi ya ulimwengu ikafichuliwa, Ee Bwana, kwa kukemea kwako, Kwa mvumo wa pumzi ya puani mwako. Alipeleka kutoka juu akanishika,*

*Na kunitoa katika maji mengi.iel na Yohana walikuwa katika eneo moja la kijiografia na wakati huohuo walikuwa eneo jingine linaloitwa katika roho. Katika roho wote wanaona mambo ambayo wakiwa katika mwili."*

**Kutokea kwenye zaburi hapo juu haya ndio tunajifunza**

- Hii ni lugha ya rohoni ambayo huonyesha mwamini akiomba katika roho kuna *vurugu* inayofanyika kutoka kwa Mungu kwenye mchakato wa kujibu maombi yake. Kwani kwa maelezo yanyotolewa kama namna ya

Mungu ya kujibu maombi ni kama hajibu kwa namna ya kistaarabu (na hapo nimetumia lugha yangu ya ulimwengu wa mwili) nae ana lugha yake kama kiumbe cha rohoni. Inawezekana kile tunachokiita vurugumechi katika kuyaitika na kuyajibu maombi, kumbe ndiyo kawaida ya mambo katika ulimwengu wa roho.

- Kama mwamini unaweza kuwa na uraia wa pande zote mbili yani raia wa rohoni na raia wa mwilini katika utendaji wako wa mambo siku kwa siku. Tazama kwa jinsi gani Mtume Yohana yupo katika mwili eneo linaitwa Patmo na yumo katika Roho.

Anaweza kutembea kwenye wamimbi ya aina hizi mbili za ulimwengu. Yupo *conversant* na ulimwengu wa mwili na wa roho! Kwa hiyo, ili unabii ueleweke kwako hauna budi kuuelewa ulimwengu wa roho, lugha yake na utumizi wa lugha huko.

- Kwa mwamini ni muhimu sana kuisikia, kuielewa na kuijua lugha ya rohoni kwa ufahamu kwamba mambo yote huanzia rohoni kuja mwilini. Hebu fikiria unaona moshi unapanda kutoka kwenye pua ya Mungu (vyovyote vile inavyomaanisha)… si utachanganyikiwa? Lazima uelewe hicho kinamaanisha nini. Na kuna maneo

yanatumika huko ndani kuelezea ni kwa kasi nan guv namna gani Mungu huja kujibu maombi.
Swali la kujiuliza, Je, Mungu ana pua? Je, ana mikono? Je, huwa ana miguu? Je, Mungu hutembea na/au kukimbia? Je, Mungu anafanana na wanadamu?
Je, maneno kama *“mkono wa Mungu”* yanamaanisha mkono kama vile ulivyo mkono wako?
Usipoelewa misamiati kama hiyo inamaanisha nini, basi unabii wote hautaeleweka kwako au utaelewa vibaya!

**Aina ya lugha za rohoni**

a) ***Lugha ya moja kwa moja***

Hii ni aina ya lugha ambayo jambo huwasilishwa kutoka ulimwengu wa rohoni kuja ule wa mwilini kwa namna na kwa lugha nyepesi ambayo mwamini huelewa moa kwa moja! Hii humaanisha kile ulichokiona ndio uhalisia wa jambo husika na kama sauti ikihusika basi humaanisha kile ulichosikika ndio uhalisia wa jambo hilo analiloliwasilisha katika ulimwengu wa rohoni na sasa limejibiwa.

Lugha hii alizungumzishwa Yusufu kwa habari ya kutaka kumuacha Mariam,

Zakaria kwa habari ya ujio wa Yohana mbatizaji, na Manoa na mke wake kwa Habari ya ujio wa Samsoni.

Walisemeshwa maneno ya moja kwa moja bila kuwa na fumbo au lugha ya picha au mfanano!

**b) *Lugha katika mfumo wa mafumbo***

Hii ni lugha ambayo kwa mpokea taarifa inamuhitaji awe na uelewa mkubwa kuhusu neno la Mungu ili kuelewa Mungu alimaanisha nini kwa kile alichokiona au kukisikia.

Mfano mzuri ni ndoto ya Farao kuhusu miaka saba ya shibe na miaka saba ya njaa

(Mwanzo 41:1-7), ndoto za Yusufu mwana wa Yakobo (Mwanzo 37:5-11) na maono aliyoonyeshwa Petro akiwa amepumzika kuhusu Kornelio (Matendo ya Mitume 10:9-16)

Unajua Farao aliota kuhusu ng'ombe saba walionona; kisha akaota ng'ombe saba dhaifu waliowameza ng'ombe wanono! Kwa mtu asiyeijua lugha ya ulimwengu wa roho anaweza asibaini kitu akaishia kusimulia mwonekano wa ng'ombe na kuhuzunika kwamba *"maskini ng'ombe wanono wameliwa!"* Kumbe kinachzungumziwa ni muda uitwao mwaka. Nani angeweza kufikiri kumbe

kwenye mawasiliano hayo, ng’ombe inamaanisha mwaka!?

Yusufu ndiyo anaota ndoto ya kwanza inayohusiana na maswala ya mashambani wakiwa wanavuna na kufunga miganda; kisha anaota ndoto kuhusu nyota na mwezi. Angeishia kuona hivyo alivyoviona basi angekosa kabisa ambacho Mungu alikuwa anawasiliana naye! Unanielewa?

Halafu Petro alipokea ndoto ya ajabu sana hususani kwa mtu kama yeye. Yuko zake kwenye maombi, amejipumzisha kisha anaona maono ya vyakula najisi na anaelekezwa kuvila. Haya ni mambo ya

ajabu sana yanaendelea kutoka ulimwengu war oho kuja wa mwilini.

Ninachokisema, mtu asipoelewa lugha ya ulimwengu wa roho, unabii utakuwa ni kichekesho kwake.

c) ***Lugha katika mfumo wa ufananisho***

Hii pia ni aina ya lugha ambayo Mungu hutumia kitu ambacho hufanana kimaumbile au rangi kumaanisha kile Mungu anakusemesha.

Mfano anaweza kukuonyesha nguo nyeupe sana lakini inadoa moja jeusi au jekundu ambalo pia linaonekana akawa inamaanisha

kuna mahali umekosea hivyo basi unahitajika mahala pa toba!

Nimejaribu kwa ufupi tu kukujengea shauku ya kujua zaidi kuhusiana na lugha ya ulimwengu war oho.

## Yaliyomo katika Unabii

*Ezekieli 37: 4,6,9,12*

*"4 Akaniambia tena, Toa unabii juu ya mifupa hii, uiambie, Enyi mifupa mikavu, lisikieni neno la Bwana.*

*6 Nami nitatia mishipa juu yenu, nami nitaleta nyama iwe juu yenu, na kuwafunika*

*ngozi, na kutia pumzi ndani yenu, nanyi mtaishi; nanyi mtajua ya kuwa mimi ndimi Bwana.*

*9 Ndipo akaniambia, Tabiri, utabirie upepo, mwanadamu, ukauambie upepo, Bwana MUNGU asema hivi; Njoo, kutoka pande za pepo nne, Ee pumzi, ukawapuzie hawa waliouawa, wapate kuishi.*

*12 Basi tabiri, uwaambie, Bwana MUNGU asema hivi; Tazama, nitafunua makaburi yenu, na kuwapandisha kutoka katika makaburi yenu, enyi watu wangu, nami nitawaingizeni katika nchi ya Israeli."*

- **Agizo la kutoa unabii**

  Kwa muktadha wa andiko, Ezekieli anaagizwa kutoa unabii. Hii ni kusema unabii hutolewa kwa maelekezo na maagizo ya Mungu mwenyewe.

  Kwenye kila unachokiona nyuma yake kuna maelekezo ya namna ya kutoa unabii; kila unachokiona kina namna yake ya kutoa unabii sio kusema vyovyote tu. Namna sahihi ya kutoa unabii inapaswa kuwa sawasawa na neno la Mungu kama vile Roho anavyomjalia kusema unabii haupaswi kuwa chini au zaidi ya neno la Mungu.

*Ezekieli 37:12SUV "Basi tabiri,* ***uwaambie, Bwana MUNGU asema hivi;*** *Tazama, nitafunua makaburi yenu, na kuwapandisha kutoka katika makaburi yenu, enyi watu wangu, nami nitawaingizeni katika nchi ya Israeli."*

- **Mwitikio wa kutoa unabii**

  *Ezekieli 37:7-8,10*

  *"7 Basi nikatoa unabii kama nilivyoamriwa; hata nilipokuwa nikitoa unabii, palikuwa na mshindo mkuu; na tazama, tetemeko la nchi, na ile mifupa ikasogeleana, mfupa kwa mfupa mwenziwe.*
  *8 Nikatazama, kumbe! Kulikuwa na mishipa juu yake, nyama ikatokea juu yake,*

*ngozi ikaifunika juu yake; lakini haikuwamo pumzi ndani yake. 10 Basi nikatabiri kama alivyoniamuru; pumzi ikawaingia, wakaishi, wakasimama kwa miguu yao, jeshi kubwa mno.”*

Kwenye andiko hilo, unabii mifupa inabaki kwenye hali ukavu na umauti mpaka pale ambapo Ezekieli ataitikia maelekezo ya kutoa unabii kama anavyoagizwa na Mungu! Ukweli ni kwamba kuna mambo mengi kwenye maisha ya mwamini yamesimama au yamekuwa katika hali za ukavu wa kudumu au ukawaida kwasababu tu mwamini hajachukua hatua ya kusema na

Maisha yake vile inavyompasa kufanya sawasawa na neno la Mungu.

Kwani *“kinywa kilichofungwa ni hatima iliofungwa”*

- **Nyakati za mshangao (nyakati za kumbe!)**

Nyakati hizi ni matokeo ya mwitikio au utii wa mwamini kwenye utendaji wa Mungu kwenye maisha yake. Unabii ni wa Mungu hivyo mtekelezaji na mdhihirishaji atabaki kuwa Yeye Mwenyewe. Hahitaji kujitahidi au bidii ya mtoa unabii! Yaani anayetamka unabii ni Ezekieli, lakini hata huo unabii ni neno la Mungu ambalo ndiyo Mapenzi yake

hivyo mtekelezaji atabaki kuwa Yeye (Mungu), Na kwa kufanya hivyo ndio nyakati za *kumbe*! humpata mwamini.

Ezekieli 37:8, “***Nikatazama, kumbe!*** *Kulikuwa na mishipa juu yake, nyama ikatokea juu yake, ngozi ikaifunika juu yake; lakini haikuwamo pumzi ndani yake.”*

Kwa kifupi, tunachokiona kwa Ezekieli hapa kwenye kipengele cha yaliyomo (contents), ni kupoea agizo (ambalo angeweza kuchagua ndiyo au hapana kutoa unabii), mwitikio wa utii ili kutoa unabii na hatimaye ndipo Mungu anakuja kwenye kuyadhirisha matokeo ambayo ameelekeza utolewe.

## Tafsiri ya Unabii

Kwenye kipengele hiki, nimekusudia kukuonyesha kati tafsiri kadhaa tulizonazo kwenye neno "unabii" kibiblia.. Tafsiri halisi ya unabii **ni kusema neno la Mungu!** Hivyo kutoa unabii ni **kuyasema mapenzi ya Mungu kwa sauti ya juu sana mithili ya muhubiri "kupaza sauti"** jambo la msingi katika kutoa unabii ni uwepo wa neno la Mungu. Likikosekana neno la Mungu, umekosekana unabii.

Ndiyo mtu anaweza akanena *"unabii"* kwa mapenzi yake yeye mwenyewe. Kimsingi, huo si unabii!

Hebu ngoja nikutazamishe jambo kwenye Maandiko Matakatifu kidogo:

2 Pet 1:21, *“**Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu;** bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.”*

Kwa msingi huo basi, unabii chanzo chake ni Mungu. Ni kwa neno la Mungu, mapenzi ya Mungu na maelekezo ya Mungu.

Kwa haraka, tazama mfano wa unabii na mapenzi ya Mungu kwenye kisa hiki cha Nabii Eliya:

1 Fal 17:1, *“Basi Eliya Mtishbi, wa wageni wa Gileadi, akamwambia Ahabu, Kama*

*BWANA, Mungu wa Israeli, aishivyo, ambaye ninasimama mbele zake, hakutakuwa na umande wala mvua miaka hii, **ila kwa neno langu**."*

Kwa harakaharaka na kwa juu inasikika kama vile mvua kunyesha au kutonyesha inategemea sana rehema za neno lake. Hata hivyo, mapenzi ya Mungu ni nini?

Kumbukumbu la Torati 11:16-17, *"Jitunzeni nafsi zenu, mioyo yenu isije ikadanganywa, mkageuka na kutumikia miungu mingine na kuiabudu; 17hasira za BWANA zikawaka juu yenu, naye akafunga mbingu kusiwe na mvua, wala nchi isitoe*

*matunda yake; mkaangamia kwa upesi mtoke katika nchi nzuri awapayo BWANA."*

Ukilisoma neno la Mungu utagundua ya kwamba mapenzi ya Mungu ni kwamba aabudiye Yeye peke yake. Alitoa maelekezo kwa taifa lake teule ya kwamba wakigeuka na kuabudu miungu mingine… mvua haitanyesha!

Mfalme Ahabu ni moja ya wafalme wabovu kuwahi kutokea kwenye historia ya Israeli Kaskazini (Samaria). Kuna ibada za miungu ziliingia na kumruhusu mke wangu, Yezebeli kuendesha maswala ya nchi.

Ni katika msingi huo wa taifa kuondoka kwenye ibada ya Mungu wa kweli, nabii Eliya anatoa tangazo ya kuwa hakutakuwa na mvua. Si kama apendavypo Yeye, hayo ndiyo mapenzi ya Mungu!

Sasa, tenga muda mzuri wa kumsoma nabii mmoja mmoja wa Agano la Kale, wote walikuwa na jambo hili la kufanana. Walitoa unabii ambao ni ama kuyafunua mapenzi ya Mungu kwa watu, kuwalekeza watu kwenye ibada ya Mungu wa kweli. Walitoa unabii kama walivyoagizwa na Mungu.

Kwa hiyo, ni sawa kusema ya kwamba unabii si kitu chochote kile ninachojisikia

kusema. Bali ni kuyafunua mapenzi ya Mungu.

Kutoa unabii sio lazima iwe juu ya mambo ya kutisha au yaliyofichika bali ni kuyasema mapenzi ya Mungu ambayo ni neno la Mungu katika uhalisia wake.

Ezekieli alitabiri kama alivyoagizwa na Mungu! Unaona kila anapotoa unabii juu ya mifupa anasema, “Bwana Mungu aiambia mifupa!”

Chukua Biblia yako! Soma! kwa sababu humo ndimo kuna mambo ya kuyatolea unabii. Humo kuna mapenzi ya Mungu.

Kwenye ulimwengu wa theolojia kuna vitu maneno mawili: *Logos na Rhema* hutumika kulielezea neno la Mungu. Wakati Logos ni neno la Mungu lililoandikwa na kutunzwa; neno Rhema ni neno lililovuviwa kwa ajili ya muda na eneo tofauti na muda na eneo la awali.

Ninachokuhimiza ni kwamba unaweza kutumia Logos au Rhema kutoa unabii!

**Vitu vya msingi sana vinavyohitajika wakati wa kutoa unabii ni;**

a) *Uwe na ufahamu -unabii*
b) *Uwe na ujasiri wa kutoa unabii*

Ufahamu (content) ya unabii ni hitaji la muhimu kabla ya kutoa unabii kwani aina hii ya content ni neno la Mungu ndani ya mtu lililo vuviwa na pia ni kwasababu ya vile mambo yanaweza kuwa au yatakavyoweza kuwa hivyo basi namna salama ya kutoa unabii ni kulisema neno la Mungu pekee.

Ujasiri utokanao na Neno la Mungu ni kifaa muhimu sana wakati wa kutoa unabii kwa

sababu unayasema mambo yasiyokuwepo kana kwamba yapo bila kujali hali au uhalisia wa jambo. Ujasiri unasaidia zaidi kwa kuwa kutoa unabii ni kwenda kinyume na mazingira au uhalisia wa jambo kwa wakati huo. Mwamini usikubali kuwa muhanga wa hali wakati ndani yako iko nguvu ya kutengeneza matokeo makubwa, amka! Anza kutabiri kinyume na hali ngumu, dhidi ya udhaifu huo ninakuona unajaa ujasiri na unaanza kulitendea kazi Neno la Bwana kwa kuanza kutabiri na Kunena kuyaelekea mambo ya maisha yako, iwe Amani kwako na watu wa nyumbani mwako.

**Kuhusu Mwandishi:**

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *‘‘Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.’’* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: [https://www.newvinechurch.or.tz](https://www.newvinechurch.or.tz)

**Mawasiliano na Mwandishi:**

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: Pastor James Kalekwa

Instagram: @pastorjameskalekwa

Youtube: Pastor James Kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

**Ratiba za Ibada**

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni

**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor ,Priscilla na Butogwa. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa

+255 754 917 764

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

MchungajiJK

+255 754 917 764

jameskalekwa.com